wakali na waharibifu inayoikabili Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, jana.

MZALENDO UK 20.

# Serikali kutoa mafunzo ufugaji samaki kibiashara

**Na MWANDISHI WETU**

SERIKALI inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji wa samaki kwa lengo la kukuza eneo hilo na kuleta tija kwa nchi na wananchi.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam juzi, na Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani (Sekta ya Uvuvi) kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Mohammed Sheikh, baada ya wizara hiyo kutia saini hati ya makubaliano kupitia Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA) na Chama Kikuu cha Wakuza Viumbe Maji Tanzania (AAT).

Profesa Sheikh alisema serikali imeweka msisitizo katika sekta za uzalishaji ikiwemo uvuvi, kwa kuweka fedha nyingi kwenye ukuzaji viumbe maji hususan ufugaji wa samaki.

"Huu ni ushirikiano kati ya wizara kupitia Chuo cha FETA kwa kuwa serikali imeweka fedha nyingi katika ufugaji wa viumbe maji. Mafunzo ya ya ufugaji wa samaki na kutengeneza mitaala inayokubalika Afrika Mashariki ni suala la msingi ," alisema Profesa Sheikh.

Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA), Dk. Semvua Mzighani, alisema mafunzo ya ufugaji samaki yatatolewa kati ya wiki moja hadi mbili, kuanzia Kampasi ya FETA iliyopo Nyegezi jijini Mwanza, ambapo walengwa ni bonde la Ziwa Victoria.

Alisema masomo yatakayofundishwa katika kozi hizo ni namna ya kupata vifaranga bora, vyakula na jinsi ya kufuga samaki.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Wakuzaji Viumbe Maji Tanzania (AAT), Dk. Charles Mahika, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwao hususan katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji chakula bora cha samaki, mafunzo ya kuzalisha vifaranga bora na upatikanaji wa masoko ya samaki.

Hati ya makubaliano hayo iliyotiwa saini kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA) na Chama Kikuu cha Wakuzaji Viumbe Maji Tanzania (AAT).

Mafunzo hayo yanafadhiliwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), kupitia Mradi wa Kikanda wa Ukuzaji Viumbe Maji (EAC TRUEFISH PROJECT).